JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

**MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26**

**DODOMA**

**Jumanne, 11 Machi, 2025**

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Kanuni ya 116 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kuwasilisha ***Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026***.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Serikali ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 yamezingatia maudhui ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na mipango mingine ya kikanda na kimataifa. Aidha, mapendekezo haya yamezingatia kikamilifu maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususani misingi iliyojengwa katika falsafa ya ***4R*** (***Reconciliation, Resilience, Reform*** and ***Rebuilding***) yaani Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Upya.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitabu cha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 kinawasilishwa katika Sura Tano. Sura *ya Kwanza* ni Utangulizi. *Sura ya Pili* ni tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi na *Sura ya Tatu* ni mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. *Sura ya Nne* ni mapendekezo ya vipaumbele na malengo na shabaha za Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 na *Sura ya Tano* ni Hitimisho.

## HALI YA UCHUMI

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Hali ya Uchumi imeelezwa katika Sura ya pili ya Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26 tulichowasilisha. Sura hii inaainisha mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia, hali ya uchumi wa kanda ya Afrika, Afrika Mashariki na mwenendo wa hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2024, pamoja na matarajio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2025. Viashiria vya

hali ya uchumi vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na hali ya ukuaji wa pato la Taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na demografia na maendeleo ya watu.

5. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Oktoba 2024 (*World Economic Outlook October 2024*), kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kuwa ndogo, ikiwa ni asilimia 3.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2023. Hakutarajiwi kuwa na mabadiliko makubwa kwa mwaka 2025 ambapo inakadiriwa kuwa uchumi wa dunia utakua kwa asilimia 3.3. Kwa mujibu wa Taarifa hii, kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa dunia inasababishwa na kuendelea kuongezeka kwa idadi ya watu wenye umri mkubwa na kupungua kwa uzalishaji katika mataifa yaliyoendelea. Sababu zingine zilizochangia kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa dunia ni kuendelea kuwepo kwa migogoro na mivutano ya kisiasa katika maeneo mbalimbali, pamoja na sera za kupunguza ukwasi hususan Marekani na Ulaya ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukabiliana na mfumuko wa bei.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.1 na asilimia 3.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.2 na asilimia 3.9 mwaka 2023, mtawalia. Kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kulitokana na kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za ukopaji katika masoko ya fedha ya kimataifa, kupungua kwa misaada na mikopo nafuu, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na migogoro ya kisiasa inayoendelea duniani, ikiwemo vita ya Ukraine. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa jumuiya hizo kinatarajiwa kufikia asilimia 5.7 kwa EAC na asilimia 4.1 kwa SADC kwa mwaka 2025.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba, 2024, mfumuko wa bei wa dunia

ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2023. Hali hii ilitokana na kuimarika kwa bei za bidhaa na huduma duniani hususan nishati. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2025. Mfumuko wa bei kwa nchi zenye kipato cha chini uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.1 mwaka 2024, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.4 mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoibuka kiuchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2023. Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2023.

8. ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa Tanzania, katika kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka 2024, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ukuaji huu ulitokana na juhudi endelevu za Serikali katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji, nishati, maji, afya, na elimu; ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi; na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara. Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 6.0 mwaka 2025 na asilimia 6.1 mwaka 2026.

9. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2024 wastani wa mfumuko wa bei nchini ulipungua na kufikia asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023. Katika kipindi kilichoishia mwezi Januari 2024, mfumuko wa bei nchini ulikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023 ikiwa ni ndani ya lengo la nchi la kubaki kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0. Aidha, viwango hivi bado viko ndani ya malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kutokuzidi asilimia 8.0 na malengo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya kuwa kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0. Kupungua huku kumechangiwa na utekelezaji wa sera thabiti za fedha, kushuka kwa bei za baadhi ya bidhaa muhimu kama vile vifaa vya ujenzi, samani za nyumbani na vitambaa vya kushonea nguo pamoja na utoshelevu wa chakula nchini.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO 2024/2025

10. ***Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Januari 2025, jumla ya programu na miradi ya maendeleo 9,711 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ikiwa ni sehemu ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Aidha, Serikali inatekeleza miradi 17 ya kielelezo yenye kulenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

    i) *Ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji*, ikiwemo ujenzi wa madaraja ya juu, ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR), ununuzi wa meli na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, na uboreshaji wa Shirika la Ndege la Taifa (ATCL)

    ii) *Ujenzi wa miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza nishati*, ikiwemo kukamilisha ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere

    *iii) Kuchochea uzalishaji wa bidhaa viwandani*

    *iv) Kukuza sekta ya madini*

    *v) Kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na utalii*

    *vi) Kukuza uwekezaji na biashara kwa kuendelea kuboresha mazingira ya biashara*

    *vii) Kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii kwa kuimarisha huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, maji, na umeme*

    viii) *Kuongeza tija katika sekta ya kilimo*

12. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango ni kama yanavyoainishwa katika jedwali hapa chini.

*Jedwali:* **Mafanikio Yatokanayo na Utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020 – 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taif awa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26**

| ***Eneo/Kiashiria*** | ***2019/20*** | ***2024/25*** | ***Lengo 2025/26*** | ***% Mafanikio*** |
|---|---|---|---|---|
| 1. Uzalishaji wa umeme (MW) | *1602.32* | ***3077.96*** | *4,915* | ***63*** |
| 2. Idadi ya vijiji vilivyounganishwa na huduma ya umeme | *8,587* | ***12,318*** | *12,318* | ***100*** |
| 3. Kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini (%) | *70.1* | ***79.6*** | *85* | ***94*** |
| 4. Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 | *556* | ***104*** | *180* | ***173*** |
| 5. Kiwango cha wanafunzi wanaomaliza DRS la VII wanaojiunga na kidato cha kwanza (%) | *48* | ***70*** | *90* | ***78*** |
| 6. Idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa TIC kwa mwaka | *207* | ***901*** | *600* | ***150*** |
| 7. Thamani ya miradi ya uwekezaji kwa mwaka (USD bilioni) | | ***8.813*** | *8.501* | ***104*** |
| 8. Kiwango cha utoshelevu wa chakula (%) | *114* | ***128*** | *140* | ***91*** |
| 9. Eneo la kilimo cha umwagiliaji (hekta) | *694,715* | ***983,466*** | *1,200,000* | ***82*** |
| 10. Idadi ya watalii | *1,035,687* | ***4,244,266*** | *5,000,000* | ***85*** |
| 11. Mapato yatokanayo na utalii (USD bilioni) | | ***4*** | *6* | ***68*** |

## MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE NA MALENGO KWA MWAKA 2025/26

13. ***Mheshimiwa Spika*****,** Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu. Aidha, Mpango unaopendekezwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa *Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26*. Hivyo, mapendekezo ya mpango yamejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

14. ***Mheshimiwa Spika*****,** mapendekezo haya ni kiungo kati ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo, Mapendekezo haya yatajielekeza katika kuainisha na kutekeleza programu na miradi muhimu ambayo haijakamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo.

15. ***Mheshimiwa Spika*****,** nguzo muhimu ya maandalizi ya Mpango ni ukuaji wa uchumi pamoja na maeneo matano ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maandalizi ya vipaumbele vya Mpango yamezingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye mapendekezo ya mpango ambavyo ni: *Ukuaji endelevu wa uchumi; kupunguza umaskini; kuzalisha ajira; kuimarishwa kwa ushindani katika masoko ya kikanda na kimataifa; maendeleo endelevu;* na *utawala bora na utawala wa sheria*. Vilevile, Mpango huu unalenga kutekeleza na kukamilisha programu na miradi ya maendeleo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali inatarajia kutenga shilingi bilioni 19,471.41, sawa na asilimia 34.1 ya Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi bilioni 57,040.25 kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,959.36 sawa na asilimia 31.7 ya

Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi bilioni 50,291.4 kwa mwaka 2024/25. Kati ya Fedha hizo, shilingi bilioni 13,320.51 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 6,150.90 ni fedha za nje kutoka vyanzo mbalimbali. Vilevile, Serikali inalenga kuongeza zaidi ushiriki na mchango wa sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia njia bunifu na mbadala za kugharamia miradi ikiwemo njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP).

17. **Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vinayopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 vimezingatia malengo tarajiwa na matokeo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Katika kuhakikisha ufanisi wakati wa utekelezaji, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele kama ifuatavyo:

i) ***Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi***: Eneo hili litajikita katika kutekeleza miradi na programu za maendeleo zinazolenga kuongeza uwezo wa nchi kikanda na kimataifa; kuimarisha utulivu na uendelevu wa viashiria vya uchumi jumla; kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara; na kuendeleza miundombinu ya usafiri na usafirishaji, TEHAMA, na nishati.

ii) ***Kuimarisha uwezo wa Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani na Utoaji Huduma*****:** Eneo hili litajielekeza katika programu na miradi ya maendeleo inayolenga kuimarisha uzalishaji viwandani.

iii) ***Kukuza Uwekezaji na Biashara*****:** Programu na miradi itakayotekelezwa katika eneo hili itajielekeza katika kuimarisha mifumo ya kitaasisi, sera na sheria za kodi ili kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji.

iv) ***Kuchochea Maendeleo ya Watu*****:** Programu na miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika eneo hili itajielekeza katika kuimarisha usimamizi na uendeshaji, mifumo na miundombinu ya elimu, afya, maji na mazingira; kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati; kukuza ujuzi kwa vijana, na kutoa mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu wa elimu ya juu.

v) **Kuendeleza Rasilimali Watu:** Eneo hili linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasimali watu nchini,

kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ili kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu ambavyo ni muhimu katika kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo.

18. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kutokomeza ugonjwa wa malaria. Hata hivyo, ugonjwa bado upo na ni moja ya magonjwa yanayoongoza kuua. Katika kuhakikisha kuwa tunatokomeza ugonjwa wa malaria, Serikali inakusudia kuanzisha kampeni maalum ya kuangamiza mazalia ya vimelea vya mbu. Bahati nzuri tunacho kiwanda kinachotengeneza dawa za kuua vimelea vya mbu hapa nchini. Serikali inakusudia kutumia dawa hizi kikamilifu kuanzia mwaka ujao wa fedha.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kama unavyofahamu katika siku za hivi karibuni kumeibuka wimbi la mataifa yaliyoendelea kupunguza au kusitisha misaada kwa nchi zinazoendelea. Serikali imeshafanya tathmini na kubaini kuwa hatua hii inatarajiwa kuathiri utekelezaji wa baadhi ya programu na miradi ya maendeleo, pamoja na huduma muhimu za jamii kama vile elimu, afya, maji, na ajira. Katika kukabiliana na changamoto hii, pamoja na hatua zingine, Serikali inakusudia kuimarisha Mfuko wa UKIMWI (AIDS Trust Fund) kwa kuufanyia mabadiliko na kuongezea fedha ili kuimarisha upatikanaji wa fedha za kugharamia matibabu ya magonjwa kama vile UKIMWI, TB, Malaria, na chanjo. Aidha, serikali inakusudia kuimarisha njia mbadala za kugharamia miradi kama vile kutumia njia za ubia wa sekta binafsi na sekta ya umma(PPP) ili kuongeza ushiriki wa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa nchi.

20. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yatajengwa katika nguzo na misingi ifuatayo:

i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi, katika nchi jirani na duniani kwa ujumla

ii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini

iii) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini

iv) Kuendelea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara

v) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko)

vi) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa

vii) Kuwa na raslimali watu iliyo bora na inayokidhi matakwa ya sasa ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu

viii) Nidhamu katika matumizi ya fedha za umma

ix) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, hususani kwa wafanyabiashara na wawekezaji wadogo na wakati wa ndani

x) Kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa mambo tuliyopanga

## HITIMISHO

21. ***Mheshimiwa Spika*****,** hakuna shaka kwamba tunaendelea kupiga hatua kubwa katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwa kuzingatia viashiria vya upimaji, mafanikio makubwa yamepatikana na yanaendelea kupatikana. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake na usimamizi thabiti wa Serikali anayoiongoza, ambayo ndiyo mtekelezaji mkubwa wa mpango huo. Aidha, ninaishukuru sekta binafsi kwa mchango wake mkubwa katika utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo. Serikali ya CCM itaendelea kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara na uwekezaji ili kuendelea kuimarisha sekta binafsi nchini.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawashukuru sana viongozi wetu wengine wakuu, Mheshimiwa Dkt. Philip Isidori Mpango, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake, na kwa usimamizi wao imara kwa sisi wasaidizi wao. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt.

Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake makini unaoleta mabadiliko makubwa na chanya Zanzibar.

23. **Mheshimiwa *Spika***, katika kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa miradi, Serikali, kupitia Tume ya Taifa ya Mipango, ilifanya *clinic* ya miradi inayotekelezwa nchi nzima ambayo matokeo yake yalibainisha kuwa kuna jumla ya miradi 9,711 inayotekelezwa nchi nzima. Mradi 7,910 ipo katika ngazi ya Sekretarieti za mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, katika kuhakikisha usimamizi thabiti na ufanisi katika utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo, tutaendelea kuhamasisha watekelezaji wa miradi kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo (National Project Management Information System- NPMIS) ili kuhakikisha taarifa za miradi na programu zinapatikana kwa wakati ,hususan wakati wa ufuatiliaji na tathmini.

24. ***Mheshimiwa Spika***, ninapohitimisha nichukue nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge wa Maswa kwa msaada wake mkubwa katika kutekeeza majukumu ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji. Vilevile ninawashukuru watumishi wenzangu wakiongozwa na Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wakuu wa taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji.

25. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipekee kabisa ninamshukuru Dkt. Mursali Milanzi, aliyekuwa Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango kwa maandalizi mazuri ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26, na kwa ushirikiano aliyonipatia katika kipindi chote alichokaimu nafasi ya Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango.

26. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba nitumie nafasi ya kumtambulisha rasmi kwa Bunge lako tukufu Dkt. Fred Matola Msemwa, aliyeteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango. Tunamkaribisha sana na tunamuahidi ushirikiano wetu wa dhati katika

kutekeleza majukumu yake mapya ya kuongoza mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

27. ***Mheshimiwa Spika*** baada ya maelezo hayo, ninaomba Bunge lako lipokee Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2025/26.

28. ***Mheshimiwa Spika**,* ninaomba kuwasilisha.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.)**,

**WAZIRI WA NCHI,**

**OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI.**

Dodoma, Jumanne 11 Machi 2025